SHERIA NA HAKI

Kwa kila Mwananchi

Iwe shauku

Toleo Na. 015 | Jarida la kila miezi mitatu | Julai - Septemba, 2013

ZLSC Yafanya Mafunzo kwa Mahakimu, Waendesha Mashtaka na Madaktari

Baadhi ya mahakimu na wanasheria wa Serikali kutoka Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka Zanzibar wakisikiliza mada inayowasilishwa kuhusu ulinzi wa Mtoto, Katika Ukumbi wa Zanzibar Beach Resort-mazizini Zanzibar tarehe 14 Septemba 2013.

KITUO cha huduma za sheria Zanzibar ZLSC kikishirikiana na Shirika la Save the Children wameandaa mafunzo ya siku mbili kwa mahakimu, Waendesha mashtaka na madaktari Unguja na Pemba.

Mafunzo hayo yaliwashirikisha Mahakimu wa mahakama Unguja na Pemba, Waendesha mashtaka wa kesi za watoto pamoja na madaktari kutoka mkono kwa mkono hospitali ya mnazi mmoja.

Mkurugenzi mtendaji wa Kituo cha Huduma za sheria Zanzibar bibi. Harusi Miraji mpatani alisema lengo la mafunzo hayo ni kuwakumbusha umuhimu wa kulinda haki za watoto na kuwafunza mbinu mbalimbali katika kutekeleza wajibu wao juu ya masuala ya watoto, pamoja na kujua sheria zinazohusiana na watoto Zanzibar.

Inaendelea Uk. 3

YALIYOMO

ZLSC yawafundisha sheria masheha polisi jamii na waratibu wanawake na watoto Pemba. Uk. 4

Hali halisi ya Haki za Watu Wenye Ulemavu Uk.8

Bunge Maalum la Katiba Uk. 16

Sheria ya Chuo cha Mafunzo Ipo katika Mchakato

KITUO cha Huduma za Sheria Zanzibar (ZLSC) kikishirikiana na Chuo cha Mafunzo Zanzibar waliandaa Mkutano wa pamoja wa kupitia Rasimu ya Chuo cha Mafunzo.

Mkutano huo ulikuwa ni wa siku mbili ambapo ulifanyika Unguja na Pemba, tarehe 20-21 Agosti kwa Unguja, na

Inaendelea Uk. 3

Baadhi ya Maafisa wa Chuo cha Mafunzo Zanzibar wakiwa makini kumsikiliza mtoa mada katika kuipitia na kuichangia Rasimu ya Sheria ya Chuo cha Mafunzo Zanzibar, katika Ukumbi wa Chuo hicho.

Jarida la Kituo cha Huduma za Sheria Zanzibar

SHERIA NA HAKI

Kwa kila Mwananchi

Ifanye haki

Iwe shauku

Toleo Na. 011 | **Jarida la kila miezi mitatu** | **Julai - Septemba, 2013**

Baaadhi ya washiriki wakifuatilia mafunzo ya Malezi Salama kwa Watoto yaliyofanyika katika Ukumbi wa Zanzibar Beach Resort, Mazizini Zanzibar.

Save the Children Yatoa Dozi ya Malezi Salama kwa Watoto

KITUO cha huduma za sheria Zanzibar kikishirikiana na Shirika la Save the Children Afrika ya Kusini wameandaa mafunzo ya siku tano kwa wadau wanaoshughulikia kesi za watoto Afrika.

Mafunzo haya yalifanyika kuanzia tarehe 23 mpaka 27 Septemba 2013 kwa ajili ya kuwafundisha wadau wa kesi za watoto njia bora za kutumia katika malezi salama pamoja na kushughulikia kesi za udhalilishaji katika ofisi za wadau hao *wanazofanyia kazi.*

Mapema Mkurugenzi Mtendaji wa Kituo cha Huduma za Sheria Zanzibar Bi. Harusi Miraji Mpatani alisema kuwa Zanzibar bado kuna wimbi kubwa la kesi za udhalilishaji wa watoto hususan kesi za kubaka ingawa Serikali kupitia Wizara ya Ustawi wa Jamii, Vijana, wanawake na watoto kwa kushirikiana na Shirika la save the Children wameandaa sheria ya Mtoto nam. 6 ya 2011 kwa lengo la kuwashughulikia ipasavyo wahusika wa kesi hizo.

Kwa upande wake muwakilishi kutoka shirika la save the Children kutoka Zanzibar Bw. Mubarak alisema kuwa mafunzo haya yamefanyika Zanzibar kwa amani na utulivu wa kisiwa hichi.

Mada zilizowasilishwa ni pamoja na nidhamu chanya (*Positive discipline*), namna ya kutatua matatizo ya watoto, kufahamu vipi mtoto anafikiri na vipi anahisi, kuweka miongozo sahihi katika kushughulikia watoto na kuweka malengo ya muda mrefu ya ushughulikiaji wa kesi za watoto.

Washiriki wa mafunzo haya walitoka katika nchi tofauti za kiafrika ambapo miongoni mwao ni Zanzibar, Kenya, Uganda, Ethiopia, Sudan, Mozambique na Zambia.

Jumla ya washiriki 30 waliopata mafunzo ya malezi salama kwa watoto ambao walitakiwa kuyatumia kwa kuwasomesha wengine wanaoshughulikia watoto pamoja na wahanga.

TUSHIKANE TUWALINDE, WALEMAVU WA AKILI

Jamii naizinduke. Iondoke makosani.
Sote natujumuike. Ulinzi uwe makini.
Idhilali iondoke. Ilindwe yao thamani.
Tushikane tuwalinde. Walemavu wa akili.

Wasitupwe peke yao. Wakainqia tabuni.
Tuwe karibu na wao. Tuwatoe mashakani.
Tuulinde utu wao. Hadhi na yao thamani.
Tushikane tuwalinde. Walemavu wa akili.

Kwa mapenzi tuwalee. Wao ni yetu sehemu.
Huduma tusimamie. Wapate yalo muhimu.
Maovu wasifanyiwe. Tujali ubinadamu.
Tushikane tuwalinde. Walemavu wa akili.

Tuzilinde afya zao. Pia na yao mavazi.
Tujue chakula chao. Tuchunqe yao malazi.
Pia usalama wao. Kulinda ni yetu kazi.
Tushikane tuwalinde. Walemavu wa akili.

Kuzijali hali zao. Huo ni wajibu wetu.
Kulinda heshima zao. Hilo ni lazima kwetu.
Huduma na haki zao. Zisichezewe na mtu.
Tushikane tuwalinde. Walemavu wa akili.

Wanafanyiwa unyama. Matendo ya Idhilali.
Kubakwa bila huruma. Idhalili yao hali.
Hebu naturudi nyuma. Hali zao tuzijali.
Tushikane tuwalinde. Walemavu wa akili.

Uzito wanabebeshwa. Wala matunzo hawana.
Watoto wanazalishwa. Ulezi uso huduma.
Mashaka wanazidishwa. Hawaonewi huruma.
Tushikane tuwalinde. Walemavu wa akili.

Wenqine hufunqwa ndani. Kama watoto wa kima.
Nje wanaitamani. Hupuuzwa wakisema.
Tuwafanyie imani. Ni watu sio wanyama.
Tushikane tuwalinde. Walemavu wa akili.

Tuzivuteni hisia. Kuwa ni watoto wetu.
Wametulazimikia. Wao ni jamii yetu.
Maovu kuwafanyia. Tunatoka kwenye utu.
Tushikane tuwalinde. Walemavu wa akili.

Serikali twaiomba. Kuliona jambo hili.
Na Mahkama sambamba. Tuwe pamoja kwa hili.
Polisi nao siyumbe. Jamii tuibadili.
Tushikane tuwalinde. Walemavu wa akili.

Taasisi binafsi. Na mashirika ya umma.
Mashekhe pia asasi. Kwa pamoja kusimama.
Tupige vita kwa kasi. Idhilali itakoma.
Tushikane tuwalinde. Walemavu wa akili.

Kama si sisi ni nani. Wa kujua utu wao.
Ni nani tawathamini. Kuzilinda haki zao.
Hima tushikamaneni. Tutambue hali zao.
Tushikane tuwalinde. Walemavu wa akili.

SAID R. HASSAN - ZLSC PEMBA.